# Ilani ya Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka

Baada ya kuidhinishwa na Msajili wa Kampuni, TAARIFA IMETOLEWA HAPA kwa Wenyehisa kwamba, kwa mujibu wa kanuni za vipengele vya sehemu ya 280 ya Sheria za Kampuni, 2015 na Hati ya Ushirika ya Kampuni, Kifungu cha 54A, Mkutano Mkuu wa Sabini na moja wa Kila Mwaka wa Kampuni ya Kenya Electricity Generating PLC utafanywa kupitia mawasiliano ya kielektroniki siku ya Alhamisi, tarehe 30 Novemba 2023 saa 5.00 asubuhi. kwa madhumuni ya kuzingatia na, ikiwa sawa, kupitisha maamuzi yaliyobainishwa hapa chini:

## Shughuli ya Kawaida

1. Kuwasilisha majina ya washirika na kutambua uwepo wa idadi ya kutosha ya wanachama kuendesha mkutano.
2. Kusoma Taarifa inayoitisha mkutano.
3. Kuzingatia na ikiidhinishwa, kupitisha Taarifa za Kifedha za Kampuni zilizofanyiwa ukaguzi kwa mwaka uliokamilika tarehe 30 Juni 2023, pamoja na Ripoti za Mwenyekiti, Wakurugenzi Watendaji na Wakaguzi waliomo.
4. Kuidhinisha malipo ya mgao wa mwisho wa mapato ya hisa wa Kshs.0.3 kwa kila hisa ya kawaida ya Kshs. 2.50, inayotolewa kodi inayoshikiliwa panapohitajika, katika mwaka wa kifedha uliokamilika tarehe 30 Juni 2023.
5. Kujadili na kuidhinisha Ripoti ya Mshahara wa Wakurugenzi Watendaji na kuidhinisha malipo ya ada za Wakurugenzi Watendaji kwa mwaka uliokamilika tarehe 30 Juni 2023.
6. **Wakaguzi:**
   Kubaini kuwa ukaguzi wa vitabu vya akaunti za Kampuni utaendelea kufanywa na Mkaguzi Mkuu au na shirika la ukaguzi atakaloliteua kwa mujibu wa Sehemu ya 23 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya 2015.
7. Kuidhinisha Wakurugenzi Watendaji kusuluhisha malipo kwa Wakaguzi.
8. **Kuchagua Wakurugenzi:**
   (i) Bi. Winnie Pertet- ambaye anastaafu kwa awamu kulingana na Kifungu cha 104 cha Hati ya Ushirika ya Kampuni na kwa kuwa anastahiki, anajitokeza kuchaguliwa tena kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni.
   (ii) Kuidhinisha Taarifa Maalum kwa mujibu wa Sehemu ya 131 na 287 ya Sheria ya Kampuni ya 2015 baada ya kupokelewa na Kampuni, nia ya kupitisha uamuzi kwamba Bw. James Opindi ambaye amefikisha umri wa miaka 70 achaguliwe tena kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni licha ya kuwa amefikisha umri kama huo, kuzingatia na ikiwa inafaa, kupitisha uamuzi ufuatao kama Uamuzi wa Kawaida:
   "Kwa Bw. James Opindi ambaye amefikisha umri wa miaka 70 na ambaye anastaafu kwa awamu na kwa kuwa anastahiki, anajitokeza ili kuchaguliwa tena kwa awamu moja kama Mkurugenzi wa Kampuni chini ya Hati ya Ushirika ya Kampuni."
   (iii) Bw. Samwel Kimani ambaye anastaafu kwa awamu kwa mujibu wa Kifungu cha 104 cha Hati ya Ushirika ya Kampuni na kwa kuwa anastahiki, hajitolei kuchaguliwa tena kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni.
   (iv) Bw. William Rahedi aliteuliwa katika mwaka wa kifedha ili kujaza nafasi ya kawaida kwenye Bodi. Anastaafu kwa mujibu wa vipengele vya Kifungu cha 104 cha Hati ya Ushirika ya Kampuni na kwa kuwa anastahiki, anajitokeza kuchaguliwa.
   (v) Bi. Josephine Koisaba aliteuliwa katika mwaka wa kifedha ili kujaza nafasi ya kawaida kwenye Bodi. Anastaafu kwa mujibu wa vipengele vya Kifungu cha 104 cha Hati ya Ushirika ya Kampuni na kwa kuwa anastahiki, anajitokeza kuchaguliwa.
   (vi) Hon. Stephen Mutai aliteuliwa katika mwaka wa kifedha ili kujaza nafasi ya kawaida kwenye Bodi. Anastaafu kwa mujibu wa vipengele vya Kifungu cha 104 cha Hati ya Ushirika ya Kampuni na kwa kuwa anastahiki, anajitokeza kuchaguliwa.
9. Kwa mujibu wa kanuni za Sehemu ya 769 za Sheria ya Kampuni ya 2015, wakurugenzi watendaji wafuatao, kwa kuwa wanachama wa Kamati ya Bodi ya Ukaguzi, Hatari na Utiifu ya Bodi wanachaguliwa kuendelea kuhudumu kama wanachama wa Kamati husika:

| | | |
|---|---|---|
| (i) | Bw. Bernard Ndungu, | Mwakilishi wa Prof. Njuguna Ndungu (Waziri - Wizara ya Fedha) |
| (ii) | Bi. Winnie Pertet | [Kutegemea iwapo atachaguliwa tena katika Bodi kulingana na kipengee cha 8(i) cha Ajenda] |
| (iii) | Bi. Josephine Koisaba | [Kutegemea iwapo atachaguliwa tena katika Bodi kulingana na kipengee cha 8(v) cha Ajenda] |
| (iv) | Bw. Stephen Mutai | [Kutegemea iwapo atachaguliwa tena katika Bodi kulingana na kipengee cha 8(vi) cha Ajenda] |

## SHUGHULI MAALUM:

10. Kuzingatia na ikiwa inafaa, kupitisha Uamuzi Maalum:
    "Kwa Makala na Hati iliyopo ya Ushirika ya Kampuni zifutwe kabisa na nafasi zao zichukuliwe na Hati mpya iliyofanyiwa marekebisho ambayo yameambatishwa kama Kiambatisho cha 1 cha uamuzi."
11. Kuzingatia shughuli nyingine yoyote ambayo taarifa yake imetolewa.

**Kwa Agizo la Bodi**



**FCS. Austin Ouko**
**Katibu wa Kampuni**

*9 Novemba, 2023*